JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI

MAFUNZO YA UENDESHAJI
WA
MABARAZA YA KATA
2016

IMEANDALIWA NA;
HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI,
KITENGO CHA SHERIA.

Toleo la November, 2018

MAFUNZO YA UENDESHAJI WA MABARAZA YA KATA - 2016

MUWEZESHAJI: Kilua, Muhsin R – Afisa Sheria[1]

1.0 UUNDWAJI NA UANZISHWAJI WA MABARAZA YA KATA

Mabaraza ya Kata yameanzishwa chini ya **Sheria ya Mabaraza ya Kata**, Namba **7** ya mwaka **1985** [*The Ward Tribunals Act, Cap 206 Revised Edition 2002*] chini ya kifugu cha **3**, ambapo kila kata lazima iwe na Baraza la Kata kwa ajili ya kusuluhisha migogoro iliopo kwenye kata husika.

2.0 WAJUMBE WA BARAZA LA KATA

(i) Muundo wa baraza

Baraza la Kata linaundwa na wajumbe siyo chini ya wajumbe **wanne** na siyo zaidi ya wajumbe **nane**. Kati ya hao wajumbe nane lazima wajumbe siyo chini ya watatu wawe wanawake kwa lengo la kuwepo kwa uwakilishi wa kijinsia.

Ni vema wajumbe wawe **nane** kwasababu, kuna muda mwingine baadhi wa wajumbe wanaweza kuwa na udhuru, kufariki au kupoteza sifa za kuwa wajumbe.

(ii) Sifa za wajumbe wa Baraza

Watu wafuatao wana sifa za kuwa wajumbe wa Baraza:-

- Awe na busara na maadili,
- Awe mkazi wa kata husika,

[1]Wakili wa Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Certificate in Law 2007-2008 IJA-Lushoto, Diploma in Law 2008-2010 IJA-Lushoto, LL.B 2010-2013 Mzumbe University, Post-Graduate Diploma in Legal Practice 2014-2015 Law School of Tanzania.

- Awe raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
- Awe na akili timamu,
- Awe na umri wa miaka 18 na zaidi. Hapa sheria haijatoa kikomo cha umri wa mjumbe. Hivyo basi busara itumike pale ambapo mtu atakua na zaidi ya miaka themanini asiteuliwe kuwa mjumbe kwani umri mkubwa una changamoto nyingi za utekelezaji wa majukumu.

Watu wafuatao hawana sifa ya kuwa wajumbe wa baraza kwa mujibu wa kifungu cha **5** cha **Sheia ya Mabaraza ya Kata**:-

- Mbunge,
- Mjumbe wa Halmashauri ya Kijiji au Kamati ya Maendeleo ya Kata "WDC",
- Mtumishi wa Serikali ,
- Mwanasheria. Kwa mujibu wa **Sheria ya Chama cha Wanasheria cha Tanganyika,** tafsiri ya Neno **MWANASHERIA** ni mtu yeyote mwenye elimu ya **SHAHADA YA SHERIA (Legum Baccaralaeus "LL.B"),**
- Mtu yeyote alie ajiriwa katika Idara ya Mahakama ya Tanzania,
- Mjumbe wa Baraza la Kijiji.

(iii) Uteuzi wa Wajumbe wa Baraza la Kata

WDC ndio chombo chenye mamlaka kisheria kuteua wajumbe wa Baraza la Kata. Wajumbe wa Baraza lazima watokane na vijijivinayo unda kata husika kwa uwiano sawa. Kila kijiji

kupitia mkutano mkuu wa Kijiji kipendekeze majina ya wajumbewatakao wakilisha Kijiji kwenye Baraza la Kata.

Baada ya wajumbe kupitishwa na mikutano mikuu ya vijijiyao, kila **Mtendaji wa kijiji**, awasilishe muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Kijiji kwa **Mtendaji wa Kata** ili usomwe kwenye kikao cha **WDC** cha kuteua wajumbe wa baraza la kata

(iv) Uteuzi wa Mwenyekiti wa Baraza la Kata

Wajumbe wa baraza la kata ndio wenye mamlaka kisheria kuchagua Mwenyekiti wa Baraza, na baadae kuthibitishwa na na WDC. Mara tu baada ya WDC kuteua wajumbe wa Baraza la Kata, wajumbe wa baraza watapewa dakika chache wakae faragha ili wachague mwenyekiti miongoni mwao na baadae jina la mwenyekiti litathibitishwa na WDC.

(v) Uteuzi wa Katibu wa Baraza la Kata[2]

Katibu wa Baraza la Kata huteuliwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi. Ni jukumu la WDC kupendekeza Jina la Katibu wa Baraza la Kata. Katibu wa Baraza la Kata lazima awe ni miongoni mwa watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi waliopo ndani ya kata, kama vile Afisa ugani, mifugo, maendeleo ya jamii, afya au mwalimu wa shule ya msingi au sekondari.

[2] Kwa mujibu wa Sheria ya Mabaza ya Kata,1985 katibu wa baraza huajiriwa toka UTUMISHI. Hivyo tokea kutungwa kwa sheria hii hakuna katibu hata mmoja aliye ajiriwa. Hivyo kwa taratibu zilizopo ni kwamba Mkurugenzi Mtendaji ni jukumu lake kuteua katibu wabaraza kwani mabaraza yote ya kata na vijiji yapo chini Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri husika.

Baada ya jina la katibu kuwasilishwa kwa Mkurugenzi Mtendaji, hatua inayofuata ni Mkurugenzi Mtendaji kuandika barua kwenda kwa katibu juu ya uteuzi. Barua itaandikwa kwa jina na cheo chake na kua na kichwa cha habari kuwa ***YAHUSU: KUTEULIWA KUWA KATIBU WA BARAZA LA KATA YA .....*** Pia barua hiyo lazima iwe na maelezo kwamba, pamoja na kutekeleza majukumu ya cheo chako cha muundo utatekeleza pia majukumu kama katibu wa baraza.

(vi) Majukumu ya Katibu wa Baraza la Kata.

Katibu wa Baraza atakua na majukumu yafuatayo:-

- ✓ Kutunza nyaraka zote za Baraza,
- ✓ Kuandika mwenendo wa mashauri,
- ✓ Kupokea mashauri yanayo letwa mbele ya Baraza, pamoja na kuyapatia namba,
- ✓ Kumtaarifu mwenyekiti wa Baraza uwepo wa mashauri mapya,
- ✓ Kupeleka Jalada la shauri pale linapo hitajika na ngazi za juu za baraza la Kata,
- ✓ Kuchapa mienendo na maamuzi ya baraza pale nakala zinapo hitajika,
- ✓ Kutoa barua za wito kwa pande zote za shauri pamoja na mashahidi wao.
- ✓ Kutunza fedha za tozo za uendeshaji wa baraza.

MOSHDC

3.0 MUDA WA MADARAKA WA WAJUMBE WA BARAZA LA KATA.

Wajumbe wa Baraza la Kata watatekeleza majukumu yao ya kusuluhisha migogoro kwa kipindi cha miaka mitatu, kwa mujibu wa kifungu cha **6(1)** cha **Sheria ya Mabaraza ya Kata**.

> ***Mfano, ikiwa wajumbe wa baraza waliteuliwa/walichaguliwa na WDC tarehe 16.08.2016 ifikapo tarehe 15.08.2019 baraza litakua limemaliza muda wake.***

Baada ya baraza kumaliza muda wake wa miaka mitatu, yale mashauri yote yalio kuwa yanaendelea yatasimama kusubiri baraza jipya. Wale wajumbe wa baraza liliopita wanaweza kuchaguliwa tena kuwa wajumbe wa baraza jipya, hii itatokana na uwadilifu wao walio uonyesha katika kipindi chao cha miaka mitatu.

4.0 NAFASI YA MJUMBE WA BARAZA LA KATA KUWA WAZI.

Nafasi ya mjumbe wa Baraza la Kata inaweza kuwa wazi, hivyo basi ni jukumu la WDC kuteua mtu mwingine mwenye vigezo vya kuwa mjumbe wa Baraza la Kata kuziba nafasi ilioachwa wazi. Zifuatazo ni sababu zinazosababisha nafasi ya mjumbe kua wazi;

(i) Kujihudhuru,
(ii) Kufariki,
(iii) Kuhama kimakazi kwenye kata nyingine,
(iv) Kuwa mjumbe wa WDC au Halmashauri ya kijiji,
(v) Kuwa mwendawazimu,

MOSHDC

(vi) Mjumbe au wajumbe watajikuta wapo kata mpya baada ya kata yao ya awali kugawanywa na ile Kata mpya imesha unda Baraza lao, nk

Mjumbe anaye jaza nafasi iliochwa wazi atatumikia nafasi hiyo kwa muda uliobakia wa uhai wa Baraza la Kata.

5.0 MAJUKUMU YA BARAZA LA KATA KIUSULUHISHI

Ni jukumu kuu la Baraza la Kata kulinda amani na utulivu kwa kuwasaidia wahusika wa mgogogro kufikia muafaka katika mgogogoro katika eneo la kata husika. Migogoro yote lazima isuluhishwe kwa njia ya kirafiki ili pande zote mbili za mgogoro zifike muafaka ili watu waishi kwa amani na upendo

6.0 MAMLAKA YA BARAZA LA KATA KIJOGRAFIA

Katika kutekeleza jukuku la usuluhishi wa migogoro, baraza la kata lita suluhisha migogoro yote iliyo jitokeza ndani ya kata husika. ***Mfano,***

1. ***"Mdai anaishi kata ya Kirua Vunjo Mashariki, mdaiwa anaishi Kata ya Kirua Vunjo Magharibi na shamba lenye mgogoro lipo Kata ya Kirua Vunjo Kusini. Hapa shauri litafunguliwa kwenye Baraza la Kata ya Kirua Vunjo Kusini pale shamba lilipo."***

2. ***"Katika Madai yasiohusu Ardhi, Mdai anaishi Kata ya Kirua Vunjo Mashariki, Mdaiwa anaishi kata ya Kirua Vunjo Kusini. Hapa mdai anaweza kufungua shauri kati Baraza la kata ya Kirua Vunjo Mashariki au Baraza la kata ya Kirua Vunjo Kusini."***

3. ***Katika Shauri la Jinai, mlalamikaji anaishi Kata ya Kirua Vunjo Mashariki, mshitakiwa anaishi Kata ya Kirua Vunjo Kusini, kosa la jinai limefanywa katika eneola Kata ya Njia Panda. Hapa shauri litafunguliwa kwenye kata ambayo kosa limefanywa (Baraza la Kata ya Njia Panda).***

Ikiwa kata imegawanywa kwa kuundwa kata mpya basi lile baraza la kata ya zamani (KATA MAMA) litakuwa ma mamlaka ya kusuluhisha migogoro ya kata mpya hadi pale kata mpya itakapo pata baraza lao la kata.

> ***Mfano; "Kata ya Kilema Kusini imegawanywa na kuzaliwa Kata mpya ya Njia Panda. Hivyo basi ikiwa ina subiriwa taratibu za kisheria kukamilika, lile baraza la Kilema Kusini litakuwa na Mamlaka ya kusuluhisha migogoro ya itakayo jitokeza katika kata ya Njia Panda hadi pale Baraza la Njia Panda litakapo anzishwa. Pia baraza la Kata ya Kilema Kusini litaendelea kusuluhisha migogogro yote inayo endelea/ilio funguliwa kabla ya Kuanzishwa kwa Kata ya Njia Panda ja.po kuwa Kata ya Njia Panda imepata baraza jipya".***

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Moshi anayo mamlaka ya kulipa mamlaka baraza la kata kususuhisha migogoro iliyopo kwenye kata nyingine.

7.0 AINA ZA MIGOGORO INAYOWEZA KUSULUHISHWA NA BARAZA LA KATA

Baraza la Kata lina mamlaka ya kusikiliza na kusuluhisha migogoro ifuatayo;

(i) Makosa/mashauri ya jinai na
(ii) Makosa/mashauri ya madai.

8.0 MAKOSA /MASHAURI YA JINAI

Baraza la Kata lina mamlaka ya kusuluhisha mashauri ya jinai,kama vile;

(i) Wizi, kama vile wa kuku, bata, njiwa na mazao.

(ii) Kotoa lugha za Matusi na vitisho. Vitisho vyenye lugha za kupelekea utendwaji wa makosa makubwa ya jinai kama vile mauaji, ubakaji, kuchoma nyumba moto na kadhalika itabidi taarifa hizo zipelekwe **POLISI**. Na Baraza la Kata halina mamlaka ya kusuluhisha.

(iii) Na makosa yote ya jinai ambayo yametajwa kwenye Sheria Ndogo za Kijiji. Hapa ina maanisha kuwa Baraza husika lazima liangalie kuwa kosa hilo limetendeka kijiji kipi kati ya vijiji/mitaa inayo unda Kata husika.

9.0 MAKOSA/MASHAURI YA MADAI

Baraza la Kata lina mamlaka ya kusuluhisha mashauri ya madai kama vile;

(i) Mikataba,
(ii) Ugoni/uzinzi,
(iii) Ndoa,
(iv) Ardhi.

10.0 NAMNA YA KUFUNGUA SHAURI MBELE YA BARAZA LA KATA

Mtu yeyote ambaye kwa uwelewa wake anaona kwamba kosa la jinai/madai limetendwa anaweza kwenda kulalamikakwa;

(i) Katibu wa Baraza la Kata au,

(ii) Mwenyekiti wa Kijiji au,

(iii) Mwenyekiti wa Kitongoji au,

(iv) Balozi wa Nyumba Kumi au,

(v) Mjumbe wa Halmashauri ya Kijiji.

Ikiwa lalamiko limepelekwa mbele ya Mwenyekiti wa Kijiji au Mwenyekiti wa Kitongoji au Balozi wa Nyumba Kumi au Mjumbe wa Halmashauri ya Kijiji, hivyo basi ni jukumu la Mwenyekiti wa Kijiji au Mwenyekiti wa Kitongoji au Balozi wa Nyumba Kumi au Mjumbe wa Halmashauri ya Kijiji kuwasilisha lalamiko hilo kwa Katibu wa Baraza la Kata.

Mlalamikaji anaweza kufungua shauri kwa njia ya***mdomo***au kwa ***maandishi***. Ikiwa ni kwa mdomo basi mpokea shauri ataliandika kwa maandishi na Mlalamikaji ataweka sahihi/dole gumba.

11.0 USIKILIZWAJI WA MASHAURI MBELE YA BARAZA LA KATA

Mara tu shauri litakapofunguliwa ni jukumu la Katibu wa baraza kulitaarifu baraza kua kuna shauri lipo mbele ya baraza. Katibu wa baraza atatoa wito wa maandishi kwa wahusika wa mgogoro kuhudhuria kwenye shauri pamoja na Mashahidi wao (kama wapo). Wito huo lazima utaje tarehe ya siku ya kusikiliza shauri pamoja na muda, aina ya shauri, sababu (chanzo cha mgogoro). Wito huo lazima uwe na maneno ya kushurutisha kuwa upande wowote ambao hauta hudhuria bila sababu za msingi, shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa maamuzi.

Ikiwa mdai hajahudhuria bila sababu za msingi basi shauri hilo litafutwa kwa gharama za mdai.

Kuna wakati ambapo mdaiwa nae ana madai dhidi ya mdai kwenye shauri hilohilo, ni jukumu la yule mdaiwa kuliomba baraza lisikilize madai hayo upande mmoja na kutolea maamuzi.

(A) PANDE ZA SHAURI KUJITOKEZA MBELE YA BARAZA

Kwa tarehe na saa iliotajwa kwenye wito, lazima pande mbili zote za shauri zijitokeze mbele ya baraza ili zitoe maelezo na kuulizwa maswali na wajumbe wa baraza namna ambayo baraza litaona inafaa.

Ikiwa mdai au mdaiwa ni***mtoto*** (mtu yeyote mwenye miaka chini ya 18) basi anaweza kuwakilishwa na mzazi wake, au mlezi, au mtu wa karibu au rafiki ambaye atamsaidia kutoa maelezo na kujibu maswali atakayo ulizwa.

WAKILI haruhusiwi kumwakilisha mtu yeyote mbele ya baraza la Kata.'***Wakili' maana yake ni Mwanasheria aliefaulu mitihani ya Shule ya Sheria ya Tanzania na kusajiliwa na Msajili wa Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ili aweze kuwakilisha wateja wake mbele ya Mahakama za Wilaya, Mkoa (Mahakama ya Hakimu Mkazi), Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mahakama ya Rufaa ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Pia wakili anayo mamlaka kisheria kuwakilisha wateja wake mbele ya***

Mabaraza mengine yalioundwa kisheria kamavile Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya, Baraza la Rufaa za Kodi, nk.

Mashauri yanatakiwa kusikilizwa katika maeneo ya wazi ili jamii iweze kusikiliza kwa maslahi ya umma. Endapo baraza litaona inafaa jamii haitaruhusiwa kusikiliza. Kuna mashauri kamavile Ndoa, shauri linalo husu mtoto na Ugoni yatasikizwa faragha.

Wajumbe wenye mamlaka kisheria (Akidi ya wajumbe) kusuluhisha / kusikiliza shauri ni kati ya Wajumbe ***Wanne*** hadi ***Nane.***

(B) USIKILIZWAJI WA SHAURI LA ARDHI

Baraza la Kata lina mamlaka ya kusikiliza na kutoa maamuzi juu ya migogoro ya Ardhi. Kifungu cha **10** cha **Sheria ya Mahakama za Ardhi,** Namba **2** ya Mwaka **2002** [*The Land Disputes Courts Act, Cap 216 R. E 2002*] kinalipatia Baraza la kata lililo anzishwa chini ya Kifungu cha **3** cha **Sheria ya Mabaraza ya Kata, 1985** mamlaka ya kusuluhisha migogoro ya ARDHI, ambayo thamani yake ya **ARDHI** au **NYUMBA** haizidi **Shilingi za Tanzania Milioni tatu (3).**

Ni jukumu la mdai kutaja thamani ya ardhi yake ili kuliwezesha baraza kujiridhisha kuwa lina mamlaka ya kusuluhisha mgogoro huo. Ikiwa mdai hafahamu vizuri thamani ya ardhi yake ni vema Katibu wa Baraza kumuuliza Mdai kua, "*Je kama ardhi yako leo hii*

*anataka kuiza, utauza shilingi ngapi?"*Kile kiasi cha fedha atakachotamka kuuza ndio itakua thamani ya ardhi.

(C) USIKILIZWAJI WA SHAURI LA NDOA

Ni jukumu la Baraza la Kata, kusuluhisha wanandoa wenye mgogoro ili waweze kushi pamoja kwa amani na upendo. Vyanzo vya migogoro ya ndoa ni; ukatili, uzinzi/ugoni, kutelekeza, utengano, au vile vitendo vyote vinavyo pelekea kuvunjika kwa ndoa.

Baraza la kata linatakiwa kujiridhisha kuwa katika mgogoro wa ndoa, ***Je ndoa hiyo ni halali mbele ya sheria za nchi?***.Kwa mujibu wa**SHERIA YA NDOA, 1971** [*The Law of Marriage Act, Cap 29 Revised Edition 2002*], Ndoa ni Mkataba kati ya mwanaume na mwanamke (wanawake) wa kuishi pamoja kinyumba kwa maisha yao yote.

Kuna aina za ndoa mbili ambazo ni ndoa za;

(i) **Mke mmoja**

(ii) **Wake wengi.** Ndoa za wake wengi zinajumuisha zile zilizofungwa kwa***Dini ya Kiisilamu*** ambapo wake hawatakiwi kuzidi wanne na ndoaza Kimila ambazo hazina ukomo wa idadi ya wake.

Namna ya kufunga Ndoa.

Ndoa inaweza kufungwa kwa;

(i) Dini: Ambazo ni zile dini zinazo tambulika Tanzania, kama vile uisilamu, ukiristo, kihindu nakadhalika.

(ii) Kimila/ ndoa za kitamaduni.

(iii) Ndoa za kiserikali/ ndoa za bomani zinazo fungwa kwenye ofisi ya Mkuuwa Wilaya.

Ni jukumu la mdai kuthibitisha kua ana Ndoa Halali kwa kuonyesha Cheti cha Ndoa, kwa ndoa zilizo fungwa kidini na kiserikali. Kwa ndoa za kimila ni jukumu la wazee wa kimila kutoa Maelezo mbele ya Baraza kuwa mdai na mdaiwa walioana kimila kwa kanuni na taratibu za kimila/utamaduni. Mila/utamaduni ni zile taratibu za kimaisha za jamii fulani ambazo zinatumika kwa muda mrefu na kukubalika na jamii hiyo ambazo hazipingani na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Sheria za Nchi ana Sera za nchi/Taifa.

Mfano;"***Mkoani Mara kuna aina ya ndoa kimila/kitamaduni inaitwa NYUMBA N'TOBO ambapo mwanamke mzee ambaye hajawahi kupata watoto au mtoto wa kiume kuoa binti. Binti huyo ataruhusiwa kutafuta mwanaume wa kuzaa nae na watoto watakao patikana ni mali ya mwanamke mzee. Aina ya ndoa hii ya kimila ni batili, kwani inakinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Sheria za Nchi na Sera za Nchi/Taifa."***

12.0 MAAMUZI YA BARAZA LA KATA KIMAHAKAMA

Maamuzi ya Baraza la Kata hutolewa kwa Wajumbe kupiga kura. Ikiwa kura za wajumbe zitalingana, Mwenyekiti wa Baraza anayo haki kisheria ya kuwa na kura ya Turufu. Mjumbe mwenye haki ya kupiga kura au kutoa maoni ni lazima awe ameshiriki katika hatua zote za usikilizwaji wa shauri.

Kwenye maamuzi ya Baraza la Kata, kila mjumbe lazima atoe maoni yake juu ya maamuzi,na maoni yake lazima yaandikwe kwenye maamuzi na kuweka sahihi yake.Maamuzi ambayo hayata kuwa na maoni ya kila mjumbe yatakua ni batili.

KATIBUwa Baraza la Kata hana haki kisheria ya kupiga kura na kutoa maoni kwenye maamuzi kwa sababu Katibu sio mjumbe wa Baraza.

Wajumbe wote wa Baraza walioshiriki kusikiliza shauri lazima waweke sahihi zao mwisho wa maamuzi pamoja na mwenyekiti. Inashauriwa ikiwa upande wa shauri utaomba nakala za mwenendo na maamuzi ya Baraza, wajumbe wasaini kila ukurasa ili kuepusha udanganyifu.

(A) SHAURI LA JINAI

Katika kusikiliza/kusuluhisha shauri la jinai, baraza la kata linaweza kutoa maamuzi yafuatayo;

(i) Upande ulioshindwa kuomba msamaha,
(ii) Kulipa faini isio zidi elfu hamsini,
(iii) Upande ulioshindwa, utekeleze mila na desturi zilizo pendekezwa na Baraza,
(iv) Kifungo cha Gerezani. Adhabu hii lazima ithibitishwe naMahakama ya Mwanzo. Baada ya mshtakiwa kukutwa na hatia, mgambo wa kata atampeleka mshitakiwa kituo cha polisi

akiwa na barua toka kwa Katibu wa Baraza kuwa mtu huyo amekutwa na hatia awekwe mahabusu akisubiri Mahakama ya Mwanzo ithibitishe adhabu. Katibu wa Baraza atapeleka jalada kwa Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Mwanzo.

(v) Upande ulioshindwa kuzuiwa kuhudhuria mikutano mikuu ya kijiji.

(B) SHAURI LA MADAI

(i) Mikataba; Katika kusikiliza/kusuluhisha shauri la madai yanayo husu mikataba, baraza la kata linaweza kutoa maamuzi /amri (zi) yafuatayo;

- Upande ulioshindwa kumlipa fidia mshindi,
- Kulipa gharama za kuendesha shauri, na
- Kutekeleza vipengele vya mkataba,

(ii) Ndoa; Katika kusikiliza/kusuluhisha shauri la madai yanahusu ndoa, baraza la kata linaweza kutoa maamuzi /amri (zi) yafuatayo;

- Wanandoa waishi pamoja kwa amani na upendo, au
- Kukataza mwanandoa mmoja kutenda matendo ambayo hayamridhishi mwenza wake, au
- Baraza kutamka kua limeshindwa kuwasuluhisha wanandoa kuishi pamoja.

(iii) Ugoni/uzinzi; Katika kusikiliza/kusuluhisha shauri la madai yanahusu ugoni/uzinzi,

MOSHDC

baraza la kata linaweza kutoa maamuzi /amri (zi) yafuatayo;

- Kulipa fidia za maumivu alio yapata baada ya mdaiwa kufanya mapenzi na mke au mume wa mdai.
- Kulipa gharama za kuendesha shauri,
- Kuamrisha mdaiwa kuto mkaribia mke au mume wa mdai.

(iv) Ardhi; Katika kusikiliza/kusuluhisha shauri la madai yanahusu ardhi, baraza la kata linaweza kutoa maamuzi /amri (zi) yafuatayo;

- Kurejesha ardhi/nyumba kwa mwenyewe,
- Kutamka mtu atimize wajibu wake ndani ya mkataba unahusisha ardhi/nyumba,
- Kuweka kizuizi,
- Kulipa fidia,
- Kulipa gharama za Shauri,
- Kugawanywa kwa ardhi.

13.0 UTEKELEZAJI WA AMRI ZA BARAZA LA KATA

A. SHAURI LA JINAI

Ni jukumu la baraza kusimamia utekelezwaji wa maamuzi yake. Ikiawa adhabu ni kifungo cha gerezani, adhabu hiyo lazima ithibitishe na Mahakama ya Mwanzo.

B. SHAURI LA MADAI

Ni jukumu la baraza kusimamia utekelezwaji wa maamuzi yake. Isipokua kwenye migogoro ya ardhi baraza la kata halina mamlaka ya kusimamia utelezwaji wa maamuzi yake. Utekelezwaji wa

maamuziyanayo husiana na ardhi lazima yathibitishwe na ***Baraza la Nyumba na Ardhi la Wilaya ya Moshi.***

14.0 RUFAA DHIDI YA MAAMUZI YA BARAZA LA KATA.

Upande wowote wa shauri ambao haujaridhika na maamuzi ya Baraza la Kata, lazima akate rufaa kwenda Mahakama ya Mwanzo ndani ya siku sitini. Isipokua;

(i) **Shauri/Madai ya Ardhi**, rufaa yake itapelekwa ***Baraza la Nyumba na Ardhi la Wilaya ya Moshi,*** ndani ya siku Arobaini na Tano **(45)**tokea siku ya kutolewa maamuzi.

(ii) **Shauri la Madai ya Ndoa**, hakuna rufaa. Hapa, Baraza la kata litatoa maamuzi kwamba Baraza limeshindwa kuwasuluhisha/kuwashawishi wanandoa kuishi pamoja.

Ahsanteni
Kwa ushauri au maoni tuwasiliane kupitia
0715/0767/0786 – 253505
kiluakilua214@gmail.com

.....MWISHO .....

MOSHIDC